**Kuchagua kwa Lutu**
**Na**
**Ellis P. Forsman**
**(The Choice of Lot)**

**Kuchagua kwa Lutu**
**Na**
**Ellis P. Forsman**
**Oktoba 14, 2011**

# Kuchagua kwa Lutu

## Mwa. 13:10-12

Mifano ya wanawake na wanaume iliyoandikwa kwenye Biblia inaweza kutoa masomo yenye thamani.
Kutoka kwa Ibrahimu tunaweza kusoma thamani ya imani kwa Mungu.
Kutoka kwa Yusufu tunaona ulinzi wa Mungu ukitenda kazi.
Kutoka kwa Ayubu tunajifunza umuhimu wa uvumilivu na imani wakati wa kujaribiwa.
Kutoka kwa Lutu, mpwa wake Ibrahimu, tunaweza kupata masomo yenye thamani katika…
Swala la kufanya maamzi.
Umuhimu wa kufanya chaguzi sahihi.
Kwanza tutaanza na utambulisho wa kuangalia maisha ya Lutu, alafu tutazame juu ya uamzi aliofanya na kwa jinsi gani ilileta faida katika maisha yake.

### Uchaguzi wa Lutu

**Katika kitabu cha Mwanzo, Lutu anatambulishwa kwetu kama…**

**Mpwa wa Abramu aliyetembea pamoja naye.**

- Mwa. 12:5, "*Abramu akamchukua Sarai mkewe, na Lutu mwana wa nduguye, na vitu vyao vyote walivyokuwa wamejipatia na hao watu waliowapata huko Harani, wakatoka ili kwenda nchi ya Kanaani; nao wakaingia katika nchi ya Kanaani.*"
- Mwa.13:1, "*Abramu akapanda kutoka Misri, yeye na mkewe, na kila alichokuwa nacho, na Lutu pamoja naye, mpaka kusini.*"

**Mtu ambaye ni sawa na mjomba wake akawa tajiri zaidi.**

- Mwa. 13:2-5, "*Naye Abramu alikuwa ni tajiri sana kwa mifungo, kwa fedha, na kwa dhahabu. Akaendelea kutoka kusini mpaka Betheli, mahali pale palipokuwapo hema yake kwanza kati ya Betheli na Ai; napo ndipo palipokuwa na madhabahu aliyofanya hapo kwanza; naye Abramu akaliitia jina la BWANA hapo. Na Lutu aliyesafiri paamoja na Abramu, yeye naye alikuwa na makundi ya ng'ombe na kondoo, na hema.*"

Kwa sababu ya muunganiko wa utajiri wa Abramu na Lutu, walilazimika kutengana.

- Mwa. 13:6-9, "*Na ile nchi haikuwatosha ili wakae pamoja; maana mali zao zilikuwa nyingi, hata wasiweze kukaa pamoja. Kukawako ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abramu , na wachunga wanyama wa Lutu; na siku zile Wakanaani na Waperizi walikuwa wakikaa katika nchi. Abramu akamwambia Lutu, basi usiwepo ugomvi, nakusihi kati ya*

*mimi na wewe, wala kati ya wachungaaji wangu na wachungaji wako; maana sisi tu ndugu. Je nchi hii yote haiko mbele yako? Baasi ujitenge nami, nakusihi; ukienda upande wa kushoto, nitakwenda upande wa kuume; ukienda upande wa kuume, nitakwenda upande wa kushoto.*"

Alipewa nafasi ya kuchagua sehemu ya kwenda, Lutu alifanya uchaguzi ambayo kwa mtazamo ulikuwa mzuri.

Mwa. 13:10-12, "*Lutu akainua macho yake akaliona bonde lote la Yordani, ya kwamba lote pia lina maji, kabla BWANA hajaharibu Sodoma na Gomora, lilikuwa kama bustani ya BWANA, kama nchi ya Misri hapo unapokwenda Soari. Basi Lutu aakajichagulia bonde lote la Yordani; Lutu akasafiri kwenda upande wa mashariki, wakatengana wao kwa wao. Abramu akakaa katika nchi ya Kanaani, na Lutu akakaa katika miji ya lile bonde; akajongeza hema yake mpaka Sodoma.*"

Lakini hataingeonekana nzuri kiasi gani, ilimsababishia Lutu huzuni na ugumu!

**Kama matokeo ya kuchagua kwake, Lutu aliadhirika…**

**Vita** – Mwa. 14: 1-12, "*BWANA akanena na Musa na Haruni katika nchi ya Misri, akawaambia, mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi kwenu; utakuwa ni mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu. Semeni na mkutano wote wa Israeli, mkawaambie siku ya kumi ya mwezi huu kila mtu kwetu atatwaa mwana-kondoo kwa hesabau ya nyumba ya baba zao, mwana-kondo kwa watu wa nyumba moja; na ikiwa watu wa nyumba ni wachache kwa mwana-kondoo, basi yeye na jirani yake aliye karibu na nyumba yake na watwae mwana-kondoo mmoja, kwa kadiri ya hesabu ya watu; kwa kadiri ya ulaji wa kila mtu, ndivyo mtakavyofanya hesabu yenu kwa yule mwana-kondoo. Mwana-kondoo wenu atakuwa hana hila, mume wa mwaka mmoja; mtamtwaa katika kondoo au katika mbuzi. Nanyi mtamweka hata siku ya kumi na nne ya mwezi ule ule; na kusanyiko lote la mkutano wa Israeli watamchinja jioni. Nao watatwaa baadhi ya damu yake na kuitia katika miimo ya miwili na katika kizingiti cha juu, katika zile nyumba watakazomla. Watakula nyama yake usiku ule ule, imeokwa motoni, pamoja na mkate usiotiwa chachu; tena na mbonga zenye uchungu. Msiile mbichi wala ya kutokoswa majini, bali imeokwa motoni; kichwa chake pamoja na miguu yake, na nyama zake za ndani. Waala msisaze kitu chake chochote hata asubuhi, bali kitu kitakachosalia hata asubuhi mtakichoma kwa moto. Tena mtamla hivi; mtakuwa mmefungwa viuno vyenu, mmevaa viatu vyenu miguuni, na fimbo zenu mikononi mwenu; nanyi mtamla kwa haraka; ni pasaka ya BWANA. Maana nitapita kati ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa nyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote Misri; Mimi ndimi BWANA.*"

**Utekaji** – mwa. 14:12, "*Wakamtwaa Lutu mwana wa nduguye Abramu, aliyekaa huko Sodoma, na mali yake wakaenda nazo.*"

**Dhuluma na mateso kutoka kwa watu wa Sodoma:**

- 2 Pet. 2: 7-8, "*Akamwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa hao wahalifu; maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao kwa kuona na kusikia, alijitesa alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku kwa matendo yao yasiyo na sheria.*"
- Mwa. 19:1-11, "*Mwezi wa tatu baada ya kutoka Waisraeli katika nchi ya Misri, siku iyo hiyo wakafika jangwa la Sinai. Nao walipokuwa wameondoka Refidimu na kufika jangwa la Sinai, wakatua katika lile jangwa; Israeli wakapiga kambi huko wakiukabili mlima. Musa akapanda kwa Mungu, na BWANA akamwita toka mlima ule, akisema, utawaambia nyumba ya Yakobo, na kuwaarifu wana wa Israeli, maneno haya; mmeona jinsi nilivyowatendea Wamisri, na jinsi nilivyowachukua ninyi juu ya mbawa za tai nikawaleta ninyi kwangu mimi. Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali yangu, nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu. Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli. Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote, BWANA aliyokuwa amemwagiza. Watu wote wakaitika pamoja wakisema , hayo yote aliyoyasema BWANA tutayatenda. Naye Musa akamwambia BWANA maneno ya hao watu. BWANA akamwambia Musa, tazama mimi naja kwako katika wingu zito ili watu hawa wasikie nitakaposema nawe, nao wapate kukuamini wewe nawe hata milele. Musa akamwambia BWANA hayo maneno ya watu. BWANA akamwambia Musa, enenda kwa watu hawa, ukawatakase leo na kesho, wakazifue nguo zoa, wawe tayari kwa siku ya tatu; maana siku ya tatu BWANA atashuka katika mlima wa Sinai machoni pa watu hawa wote.*"

**Kupoteza utajiri wake wote wa kimwili:**

- Mwa. 19:15-16, "*Hata alfajiri ndipo malaika wakamhimiza Lutu, wakisema ondoka mtwae mkeo na binti zako wawili waliopo hapa, usipotee katika maovu ya mji huu. Akakawia-kawia; nao wale watu wakamshika mkono, na mkono wa mkewe, na mkono wa binti zake wawili, kwa jinsi BWANA alivyomhurumia, wakamtoa wakamweka nje ya mji.*"
- Mwa. 19:24-25, "*Ndipo BWANA akanyesha juu ya Sodoma na Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa BWANA. akaangusha miji hiyo na bonde lote, na wote waliokaa katika miji hiyo, na yote yaliyomea katika nchi ile.*"

**Kifo cha mkewe:**

- Mwa. 19:17, "*Ikiwa walipomtoa nje, mmoja alisema, jiponye nafsi yako usitazame nyuma, wala usisimame katika hilo bonde popote; ujiponye mlimani usije ukapotea.*"
- Mwa. 19:26, "*Lakini mkewe Lutu akatazama nyuma yake, akawa nguzo ya chumvi.*"

Mfano wa Lutu unatakiwa utuvutie kutokana na umuhimu wa kuchagua sahihi katika maisha yetu. Kwa mtazamo wa kile kilichomtokea Lutu, sasa tutaangalia…

Baadhi ya uchaguzi tunaofanya ambao uathiri maisha yetu kwa sehemu kubwa. Baadhi ya mapendekezo ya namna gani tunapaswa kufanya uchaguzi sahihi. Ni nini cha kufanya tunapogundua tumefanya uchaguzi mbaya.

Hivyo zingatia…

**Chaguzi zetu**

**Ni uchaguzi upi tunaoufanya ambao huathiri maisha yetu kwa sehemu kubwa?**

**Ambayo itaathiri maisha yako zaidi ya kitu kingine: Kuchagua kumfuata Yesu!**

Itaamua sehemu yako katika umilele.

Itacchukuliana katika kila uchaguzi unaofanya; maana kama mfuasi wa Kristo utajali kufanya mapenzi yake, siyo yako mwenyewe.

**Kuchagua kazi yako.**

Uchaguzi unaofanya unaweza ukawa na madhaara ya mwisho juu ya ndoa yako, familia na huduma yako kwa Mungu.

Hata katika mtazamo wa kidunia, uchaguzi wako ni muhimu, maana soko la kazi linaweza kubadilika sana.

**Kumchagua mweza wako.**

Uchaguzi unaofanya unaweza ukawa mzuri hata katika kiwango chako cha furaha katika maisha haya.

Itakuwa na uzao wa muda wote wa watoto na uimara wa hisia zao.

**Kuchagua marafiki zako.**

Kuwa na marafiki wa karibu inaweza ikawa baraka ya ajabu.

Mit. 17:17, "*Rafiki hupenda siku zote; na ndugu amezaliwa kwa siku ya taabu.*"

Lakini rafiki wabaya wanaweza kuwa laana kwa wenye haki.

- Mit. 12: 26, "*Mwenye haki ni kiongozi cha mwenzake; bali njia ya wasio haki huwakosesha.*"
- 1 Kor. 15:33, "*Msidanganyike, mawazo mabaya huaribu tabia njema.*"

**Kuchagua sehemu ya kuishi.**

Ilikuwa ni katika kuchagua huku ndipo Luta alifanya kosa.

Wanaweza kuwepo “Sodoma” ya kisasa na “Gomora”!

**Tunawezaje kufanya uchaguzi sahihi zaidi?**

**Muombe Mungu akupe hekima.**

Yak. 1:5-8, “*Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima na aombe dua kwa Mungu awapaye wote, kwa ukarimu wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani pasipo shaka yoyote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwaa na upepo na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote.*”

**Tafuta ushauri kwa wengine.**

- Mit. 11:14, “*Pasipo shauri taifa huanguka; bali kwa wingi wa wokovu huja wokovu.*”
- Mit. 12:15, “*Njia ya mpumbavu imenyoka machoni pake mwenyewe; bali yeye aliye na hekima husikiliza shauri.*”

Ongea mambo yako na wengine, Wakristo waliokomaa.

Uliza hekima ipatikanayo katika Biblia (hasa katika kitabu kama Mithali).

**Chochote ufanyalo, ifanye kwa ajili ya Bwana.**

- Zab. 37:5-6, “*Umkabidhi BWANA njia yako, pia umtumaini, naye atafanya. Ataitokeza haki yako kama nuru, na hukumu yaako kama adhuhuri.*”
- Zab. 37:23-26, “*Hatua za mtu zaimarishwa na BWANA, naye aipenda njia yake. Ajapojikwaa hataanguka chini, BWANA humshika mkono na kumtegemeza. Nalikuwa kijana nami sasa ni mzee, lakini sijaona mwenye haki ameachwa wala mzao wake akiomba chakula. Mchana kutwa hufadhili na kukopesha, na mzao wake hubarikiwa.*”
- Yak. 4:15, “*Badala ya kusema Bwana akipenda, tutakuwa hai na kufanya hivi au hivi.*”

**Tunafanyaje tukigundua kwamba uchaguzi wetu hauko sahihi?**

**Fanya alichokifanya Lutu:**

Sikiliza neno la Mungu (kama kuikimbia Sodoma na Gomora).

Fanya kilicho sahihi pasipo kumbukumbu (kumbuka mke wa Lutu!).

**Fanya alichokifanya Petro baada ya kumkana Kristo:**

Tubu, kama kuna dhambi imehusika katika uchaguzi uliofanya.

Rudi katika kumtumikia Bwana.

**Fanya kile alichokifanya Paulo baada ya kulitesa kanisa:**

Kubali msamaha anaoutoa Yesu.

Amua kuishi kwa ajili ya Bwana maisha yako yote kwa kadiri ya uwezo wako.

Kitu kibaya cha kufanya ni kuendelea kuwa katika uchaguzi mbaya kwa sababu ya kiburi au sababu nyingine! (hata kama kuna baadhi ya chaguzi tunapaswa kuishi navyo).

## Hitimisho

Mfano wa Lutu unaweza kutumika…

Katika kutufundisha kwamba kufanya maamzi sahihi ni muhimu.

Kutuonya tusifanye maamzi rahisi.

"mkumbuke Lutu" wakati mwingine unapokumbana na maamzi muhimu.

Tafuta kufanya maamzi yanayoendana na mapenzi ya Bwana na siyo yako mwenyewe.

Hatima yako ya milele (na ya wale uwapendao) inaweza kutegemea uchaguzi wako.

Je umefanya maamzi muhimu zaidi ambayo hutakumbana nayo kamwe? Uamzi wa kumfuata Yesu kama Bwana na Mwokozi? Kama bado, kwa nini isiwe leo? Unapaswa kufanyika Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb.11:6*, "Maana pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana yeye ajye kwa Mungu lazima aamini kwamba yeye ndiye, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17) kijana mmoja jirani yangu miaka sawa na ya kwangu aliniambia kuwa aamini katika Mungu. Kwa vile nilikuwa nimebatizwa, nikachukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamab kuna Mungu. Lakini ilikuwa sehemu yenye usalama, niheri aende kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) katika siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu atamuruhusu aingie mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.
- **Toba.** Matend. 2:38*, "Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend 11:18*, ".....Mungu amewajalia hata mataifa nao toba iletayo uzima."* Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba nyingine, ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi humu ndani!" Na unachukua simu yako na kuwa pigia polisi, ukiwambia kuwa kuna mwizi nyumbani kwako. Muda mfupi unasikia wanafika na kumshika mwizi. Anapiga kelele,

“samahani; samahani!” Anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi lazima aombe msaha kwamba hataiba tena na kubadilisha maisha yake. Ni badiliko la nia linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kufanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10*, “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.”* Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba kifungu hicho kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni “**KATIKA**” haki, uzima au wokovu. “Katika” inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba tayari amesha pata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote, “*Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa. Kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akambatiza. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye.”* (Math. 3:14-17).

Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema “imekuwa kwetu **sisi** “*kuitimiza haki yote*” Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tungali katika dhambi zetu. *“Petro akawambia tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu*.” (Matend. 2:38). Petro, umesema ni nini maana ya ubatizo? “kwa ajili ya ondoleo la dhambi.” Kwa nini yeyote anaweza kuacha hatua inayotuondoa dhambi?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tuzikwe. “*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.”* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Paulo (kabla hajaitwa Paulo) kitu kile kile *“Sasa unakaawilia nini? Simama, na ubatizwe ukaoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana.”* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. *“Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na*

*sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* ( Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani yake Mungu kwa kupaka damu yake Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tuko huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuziki mwili kaburini kwa kuweka udongo mdogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa Mkristo, kwa nini usizingatie leo?